Kukagua Matokeo

Ili msaada wa kifedha uwe na maana, ni sharti uwe na matokeo ya kudumu na tena zenye kuthibitika.

Ustawi Ukaguzi

Wafadhili wanataka thibitisho kwamba fedha zinazotolewa na walipa kodi zinaleta matokeo, na wanaopokea fedha wanapenda kuona mabadiliko ya maana katika hali ya maisha yao.

Ustawi wa Misaada

Katika mwaka wa 2002 Benkik ilifanya utafiti wa taathiri ya misaada ya maendeleo ya nusu karne iliyopita. Kulingana na ripoti ya mwisho, The Role and Effectiveness of Development Assistance: Lessons from World Bank Experience (663k pdf) [Umuhumi na Taathira za Misaada ya Maendeleo: Mafunzo kutokana na maarifa ya Benki ya Dunia], maendeleo kwa jumla yamekuwa ya yakupendeza sana kwa mda huu:

- Katika miaka 40 ilyopita, kadirio la maisha wakati wa uzazi katika nchi zinazoendelea limeongezeka kwa miaka 20.
- Katika miaka 30 ilyopita, kutojuwa kusoma na kuandika kumepunguzwa kwa karibu nusu kutoka asilimia 47 hadi asilimia 25 ya watu wote wazima katika nchi zinazoendelea.
- Katika karne mbili zilizopita idadi ya watu wanaoishi katika ufukara wa juu zaidi (umeelzwa kuwa hali ya kuishi kwa pato la chini ya $1 kwa siku) imeanza kupungua hivi sasa—kwa kama watu milioni 200—baada ya kuongezeka katika karne za 19 na 20.

Maendeleo haya yamesabibishwa na kuongezeka kwa kiwango cha kukua katika nchi zinazoendelea. Kwanza mwaka wa 1990 tu, uchumi wa nchi zinazoendelea umekua kwa jumla ya kiasi kikubwa zaidi cha pato lake la jumla kupita ule wa nchi za Organisation for Economic Co-operation and Development (OECD) [Muungano wa Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo]—kwa kiasi cha 1.9 dhidi ya 1.6 kwa mia. Hii hasa ni kwa sababu ya sera bora zaidi, pamoja na masoko yenye nguvu zaidi ambayo yamesababisha kuwa na mazingira bora zaidi ya kukuza sekta ya kibinafsi katika nchi nyingi. ***Maendeleo katika afya, elimu, na mapato siyo kwa bahati.*** Kwa sababu ya usaidizi kutoka kwa jamii ya maendeleo na mashirika ya huduma za umma, serikali zimeharakisha kukua na kupunguza umasikini kwa kuboresha sera zao, taasisi zao, serikali, na kwa kupitia miradi na programu zilizoandaliwa vyema. Lakini maendeleo haya hayajakuwa ya sawa kwa pande zote na yanaweza kuhadaa. Hata hivyo, msaada wa maendeleo haijastawi vyema. Sehemu ya Afrika haijakuwa na ongezeko katika kiasi la pato lake la jumla kati ya mwaka wa 1965 na 1999. Ukimwi umepunguza kadirio la maisha katika Afrika kusini mwa Sahara kwa miaka mitatu katika miaka ya 1990, na kiasi cha mapato ya watu kwa sehemu ya Afrika hakijaongezeka tangu mwaka wa 1965. Uchumi katika nchi nyingi za Ulaya ya Mashariki na Asia ya Kati imeathiriwa na ongezeko kubwa la umasikini katika miaka ya 1990.

Penye hatua njema za maendeleo, sifa huenda kwa hatua za nchi zenyewe haswa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na pia katika kuwekeza katika wananchi. Wakiwa na ufahamu huu, wafadhili kwa sasa wamekuwa wakipeleka rasilimali zao kwa mageuzi na kuimarisha halimashauri. Utafiti wa Benki ya Dunia umethibitisha kwamba umasikini haupunguziki kwa kufwatilia mwenendo wa mipango ya kati iliyofwatwa na nchi nyingi miaka ya 1950 na 1960, wala sio kwa mipango kiasi ya serikali ya soko huru iliyotiliwa mkazo na watu wengi katika miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990. Ili kuwe na mafanikio, nii muhimu kuwe na hatua za pamoja kutoka kwa nchi matajiri. Sehemu moja muhimu ni ile ya sera za biashara, kwa sababu nchi masikini ndizo zenye kuumia zaidi kwa hatua za nchi matajiri kujipendekezea mapato ya biashara kwa kuwekewa kodi maradufu kwa bidhaa zao ukilinganisha na bidhaa kutoka nchi matajiri.

Msaada wa maelewano wa Benki ya Dunia ni wa manufaa katika kupunguza umasikini. Misaada ya kifedha ya IDA, ambayo inaelekezewa nchi masikini imeonekana kuwa na mafanikio mema zaidi: ina mafanikio wa asilimia 50 zaidi kushinda official development assistance (ODA) [msaada rasmi wa maendeleo]. Msaada unaoelekezwa vyema huongeza uwekezaji wa kibinafsi wa ndani ya nchi na wakigeni pia kwa kutia nguvu mipango iliyoimarishwa pamoja na kusaidia kuimarisha miradi ya ustawishaji, halmashauri, na wanavyohitaji waweka hazina. Utafiti inaonyesha kwamba kila dollar moja ya IDA inaleta ongezeko la karibu dollar mbili ya uwekezaji wa jumla, zikiwemo senti 60 za foreign direct investment (FDI) [uwekezaji wa kigeni].

Shughui za Benki pia zina manufaa katika sehemu za afya na elimu. Benki ndiyo mfadhili mkubwa zaidi wakigeni wa elimu. Kwa jumla imepeana bilioni $30 kwa miradi ya elimu. Na pia ni mfadhili kubwa zaidi ulimwenguni wa miradi ya afya, ikiwa na miradi ya thamani ya bilioni $1.3 kwa mwaka kwa afya, lisho bora na miradi yaumma. Miradi hii ilikuwa na matokeo mema na mara kadhaa iliigizwa katika sehemu nyengine kando na penye miradi.

- Uchina kwa mfano, mradi wa mwishoni mwa miaka ya 1990 ulisaidia kuongeza idadi ya jamii zinazotumia chumvi yenye madini kutoka asilimia 40 hadi 89, na kupunguza upungufu wa madini ya iodine katika marika yaliyofanyiwa utafiti kutoka asilimia 13 hadi 3. Mwishowe, husababisha ongezeko la alama 10 hadi 15 katika viwango vya IQ za watoto katika jamii zilizo athiriwa.
- Nchini Mali, mradi wa mapema katika ya 1990 ulisaidia kuongeza kiasi cha watoto waliyopata chanjo kamili kutoka ailimia 0 hadi 24.
- Katika sekta ya elimu, kusajilishwa watoto wa kike Bangladeshi kumeongezeka kwa kadri — kutoka asilimia 34 ya walioko shule ya upili katika mwaka 1990 hadi asilimia 48 mwaka wa 1997 — kukiweko na usaidizi wa mradi wa Benki.

Uadilifu na wasia ni muhimu kama fedha. Ingawa Benki ya Dunia inajulikana vyema zaidi kwa kuwa mfadhili wa kifedha, moja ya shughuli zake muhimu ni huduma ya uadilifu na wasia ambayo ni muhimu sana kwa kuboresha sera za kudumu zenye kusaidia kukuza uchumi na kupunguza umasikini.
Katika nchi nyingi, rasilimali haitoshi ili fedha pekee yake ilete mabadiliko kulingana na uthibiti. Mashirika ya kimataifa ya fedha pamoja na wafadhili wengine yanapoleta maendeleo mema, ni kwa sababau usaidizi wao umepita zaidi ya upatianaji wa rasilimali bali umesaidia nchi kufanya mabadiliko muhimu iwe ni katika kutekeleza ujenzi wa halmashauri ama kwenye kusambaza miradi ya majaribio. Katika nchi sita, Benki imefanya uvumbuzi wa mchango muhimu uliopatikana kwa usaidizi wa wafadhili wengine, kupitia uadilifu na wasia, pamoja na msaada wa kifedha ambao umekuwa wenye umuhimu mkubwa kwa mabadiliko yanayo tekelezwa na nchi zenyewe kama: Uchina, India, Mozambique, Uganda, Poland, na Vietnam.

Matokeo: Benki, pamoja na jamii yote ya wafadhili imetilia mkazo matokeo ilikuweza kufikia malengo ya MDG kwa wakati ufaao. Matokeo hayapatikani pasipokuwa na uhakika, na kujumuisha malengo na shabaha. Pamoja na juhudi zake za kuendeleza miradi, Benki inaanda kuanzisha mpango wa usimamizi wa pande zote ulimwenguni ili kutalii viasheria na maendeleo ya kufikia malengo ya MDG.
Kuhusiana na International Development Association [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo], fedha zilizopeanwa na wafadhili kwa kufidia akiba ya mchango wa marekebisho wa Julai 2002 zilikuwa sambamba na usimamizi na ukaguzi pamoja na kuangalia matokeo, vyote ambavyo vimeleta mwelekeo wa results-based Country Assistance Strategy [Mpango wa usaidizi kwa Nchi Kulingana na Matokeo].
Lakini namna za kupimia matokeo zinawekewa miradi yote ya Benki. Ili mradi ukubaliwe na Bodi za Wakurugenzi, ni wajibu mradi uwe na mwelekeo wa Millennium Development Goal [Shabaha ya Karne ya Maendeleo] ama moja ya mipango halisi ya Benki. Wakati huohuo, Takwimu za miradi ya Benki imepangwa kwa mada.
Ukaguzi na Makadirio ya Juu
Benki ina miradi kadhaa ya ndani na nje ya kujikagua.

- Ulio mkubwa na wa kale zaidi ni Operations Evaluation Department [Idara ya Uendeshaji wa Ukaguzi], iliyobuniwa miaka 30 iliyopita. Idara hii hutoa ripoti ya shughuli za Benki kwa nchi wanachama. Matokeo ya miradi, kama ilivyokauguliwa na Idara ya Uendeshaji wa Ukaguzi iliyo huru ya Benki ya Dunia, imekuwa imara zaidi kwa mda wa karne iliyopita. Mbali na kukua na kupanuka kwa agenda ya maendeleo, Benki imeongeza kiwango cha miradi iliyobainishwa kuwa yakuridhisha ambayo imefaulu kufikia shabaha za miradi kutoka asilimia 60 mwishoni mwa miaka ya 1980 hata ikapita asilimia 80 hivi leo.

- Mwaka wa 1993, wanachama walibuni baraza huru la ukaguzi ili kushughulikia maswala ya watu wanaoathiriwa na miradi ya Benki na kuhakikisha kuwa mipango ya usalama inatekelezwa.

- Tofauti na OED, ambayo hufwatilia miradi baada ya kukamilishwa, halmashauri ya ndani Quality Assurance Group (QAG) [Mchangano wa Kuhakikisha Usawa] huikagua wakati wa utekelezaji ambapo mabadilko yanaweza kendelea kufanywa. Internal Auditing Department [Idara ya Uhesabu wa Ndani] hushughulikia usimamizi wa athari na uelekezi wa ndani. Idara hii hufanya kazi kulingana na Standards for the Professional Practice of Internal Auditing of the Institute of Internal Auditors [Maelekezo ya Utaalamu wa Uhandisi wa Ndani wa Kitivo cha Uhandisi wa Ndani].

- Novemba mwaka wa 2000 Corporate Committee on Fraud and Corruption Policy [Kamati ya Uendeshaji dhidi ya Udanganyifu na Ufisadi] ilibuniwa kuhakisha kwamba Bank Group [Mshikano wa Benki] unaanzisha sera dhidi ya ufisadji na kubuni namna za kupunguza umasikini. Nayo kituo dhidi ya udanganyifu na ufisadi kwa sasa inajulikana kama Department of Institutional Integrity (INT) [Idara ya Uaminifu wa Ushirika]. INT huchunguza shutuma zote za udanganyifu na ufisadji katika Mshikano wa Benki ama iliyohusiana na kandarasi zilizo fadhiliwa na Benki pamoja na kuchunguza shutuma au madai yoyote ya tabia kwa wafanyakazi isiyokuwa ikiambatana na mipango ya Benki. Mbali na hayo, Ethics Office [Ofisi ya Usimamizi Mwema] hutoa ripoti kwa Rais wa Benki na inajukumu la mawasiliano juu ya mambo haya.

- Katika mwaka wa fedha wa 2001 Benki ilibuni Quality Assurance and Compliance Unit in its Environmentally and Socially Sustainable Development [Kuhakikisha kwa Usawa na Kuambatana na Maendeleo Salama kwa Mazingira na Jamii] ili kuhakisha kuwa utekelezaji wa sawa wa hatua za usalama, kama vile sera ya watu waliyo wenyeji wa asiliama mpango wa kuhamishwa fasi na kufidiwa, na kutoa wasia juu ya hatua za usalama katika miradi.